

Date Printed: 04/23/2009

---

JTS Box Number: IFES\_73  
Tab Number: 7  
Document Title: Uchaguzi Mikuu 29 Octoba 1995  
Document Date: 1995  
Document Country: Tanzania  
Document Language: Swahili  
IFES ID: CE01892




\* F E A 6 1 E 3 5 - 3 7 F 7 - 4 0 2 E - 8 B 8 B - 4 7 7 E 9 8 A 6 A B 9 5 \*

**UCHAGUZI MKUU**  
**29 OCTOBA, 1995**



**TUME YA TAIFA YA**  
**UCHAGUZI TANZANIA**  
**S.L.P.10923,**  
**DAR ES SALAAM.**

- \* UCHAGUZI HUU NI WA  
VYAMA VINGI VYA SIASA.
- \* VYAMA VYOTE VINA HAKI  
SAWA KATIKA UCHAGUZI  
HUU.



- \* UNA UHURU WA  
KUMCHAGUA MGOMBEA.  
YEYOTE UNAYEMTAKA  
BILA HOFU; KURA NI SIRI  
YAKO.
- \* UNA HAKI YA KUPIGA  
KURA HATA KAMA SI  
MWANACHAMA WA  
CHAMA CHOCHOTE.


**\* TUNZA SHAHADA YAKO  
YA KUANDIKISHWA HADI  
MWISHO WA UCHAGUZI.**

**\* USIUZE WALA KUMPA  
MTU MWINGINE  
SHAHADA YAKO.**



**\* WALEMAVU, WASIOONA  
NA WASIOJUA KUSOMA  
NA KUANDIKA WANAYO  
HAKI YA KUPIGA KURA,  
NA WATASIDIWA  
KUFANYA HIVYO.  
SIKU YA UCHAGUZI KILA  
ANAYEHUSIKA ANAWEZA  
KWENDA KITUONI NA  
MTU WA KUMSAIDIA  
KUPIGA KURA YAKE.**

- \* UKIANDIKISHWA KUPIGA KURA, UNA HAKI YA KUMDHAMINI MGOMBEA MMOJA WA CHAMA KIMOJA CHOCHOTE KWA UCHAGUZI WA RAIS NA MAKAMU, NA MGOMBEA MMOJA KWA UCHAGUZI WA BUNGE.



- \* KAMA WEWE NI MGOMBEA UNA HAKI YA KUPINGA KWA MAANDISHI UTEUZI WA MGOMBEA MWINGINE AMBAYE HAKUTIMIZA MASHARTI.
- \* KAMA WEWE NI MGOMBEA NA HUKURIDHIKA NA UAMUZI WA MSIMAMIZI WA UCHAGUZI KUHUSU PINGAMIZI, UNA HAKI KUKATA RUFAA KWA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI.

**\* UNA HAKI YA  
KUHUDHURIA MIKUTANO  
YA KAMPENI YA CHAMA  
CHOCOTE. SIKILIZA KWA  
MAKINI ILI UELEWE SERA  
ZA VYAMA HIVYO. ULIZA  
MASWALI KWA UTULIVU.**




**\* WASIKILIZE WAGOMBEA  
WA VYAMA MBALIMBALI  
HATA WAKUJA NYUMBANI  
KWAKO.**

**\* UPIGAJI KURA NI TAREHE  
29 OKTOBA, 1995.**

**\* KAMPENI YA AINA  
YOYOTE SIKU YA KUPIGA  
KURA NI UVUNJAJI WA  
SHERIA.**

**\* WAHI KWENDA KITUONI  
UKIWA NA SHAHADA  
YAKO YA KUANDIKISHWA.**

**\* ONYESHA SHAHADA  
YAKO KWA MSIMAMIZI  
WA KITUO ILI UPATE  
KARATASI ZA KUMPIGIA  
KURA RAIS NA MBUNGE.**



**\* NENDA SEHEMU  
ILİYOTENGWA WEKA  
ALAMA HII ✓ NDANI YA  
CHUMBA CHINI YA PICHA  
YA MGOMBEA  
UNAYEMTAKA.**

**\* USIANDIKE CHOCHOTE  
KINGINE KWENYE  
KARATASI YA KURA  
VINGINEVYO KURA YAKO  
ITAKUWA IMEHARIBIKA.**

Country TANZANIA

Year 95 Language Ki Swahili

Description VOTER ED- STEPS

(Natl Electoral Commission)

IFES developed/sponsored? \_\_\_\_\_

VYAMA VINGI TAIFA MOJA